



**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**  
**WIZARA YA AFYA**  
**BARAZA LA FAMASI**



## **TAARIFA KWA UMMA**

### **KUSITISHA KUTAMBULIWA KWA WATOA DAWA WA KOZI YA MWAKA MMOJA (ONE YEAR PHARMACEUTICAL DISPENSERS)**

**DODOMA: 22 Mei, 2026**

Baraza la Famasi ni taasisi ya Serikali iliyopo chini ya Wizara ya Afya, iliyoanzishwa kwa mujibu wa Kifungu cha 3 cha Sheria ya Famasi, [Sura 311, Marejeo ya 2023]. Pamoja na majukumu mengine Baraza limepewa jukumu la kusajili wanataaluma wa kada ya famasi na kusimamia maadili na utendaji kazi wao.

Katika kikao cha Baraza cha 57 kilichofanyika tarehe **19–20 Agosti, 2025**, iliamuliwa kusitisha utambuzi wa wahitimu wa kozi ya mwaka mmoja ya utoaji dawa (*One-Year Pharmaceutical Dispensers*). Hivyo, Ofisi ya Msajili inapenda kuutaarifu umma kuwa utambuzi wa watoa dawa wa kozi ya mwaka mmoja utasitishwa rasmi kuanzia tarehe **01 Desemba, 2026** kwa kuzingatia utaratibu ufuatao:

**(a) Kusitishwa kwa Mitihani ya Usajili na Taaluma kwa Watoa Dawa wa Kozi ya Mwaka Mmoja**

Watoa dawa wa kozi ya mwaka mmoja wataruhusiwa kufanya **Mitihani ya Usajili na Taaluma** hadi kufikia mwezi Novemba, 2026. Baada ya hapo, mitihani hiyo kwa wahitimu wa kozi ya mwaka mmoja itasitishwa rasmi. Watoa dawa ambao hawatakuwa wamefaulu mitihani hiyo ndani ya muda uliowekwa watatakiwa kujiendeleza kielimu hadi kufikia angalau ngazi ya Astashahada (*certificate*) au zaidi ili waweze kutambuliwa na Baraza.

**(b) Watoa Dawa Wanaotambuliwa na Baraza kwa Sasa**

Watoa dawa wote ambao tayari wanatambuliwa na Baraza wataendelea kusimamiwa kama wanataaluma wengine waliosajiliwa. Pia watatakiwa kuhuisha taarifa zao kila mwaka kwa mujibu wa taratibu zilizowekwa. Baraza litaendelea kuwajengea uwezo wa kitaaluma kupitia mfumo wa Mafunzo Endelevu ya Kitaaluma (*Continuing Professional Development - CPD*) ili kuhakikisha utoaji bora wa huduma za afya kwa wananchi.

**(c) Wanafunzi Wanaotarajia Kuhitimu kama Watoa Dawa**

Wanafunzi walioko vyuoni wanaotarajia kuhitimu kama watoa dawa wa kozi ya mwaka mmoja, kuanzia tarehe 01 Desemba 2026, watapaswa kuendelea na masomo yao hadi kufikia ngazi ya astashahada au zaidi ili waweze kusajiliwa na Baraza.

**Imetolewa na:**  
**Msajili - Baraza la Famasi**  
**S. L. P. 1277, Dodoma**  
**Barua pepe: [info@pc.go.tz](mailto:info@pc.go.tz)**  
**0800110015**